## HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA USIMAMIZI NA URATIBU WA MIRADI YA UVIKO - 19 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI TAREHE 22/10/2021

### 1.0 MAHUDHURIO

### 1.1 WAJUMBE

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Japhet Haule | - | Afisa Afya | - | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Elias Mafwele | - | Mchumi | - | Katibu |
| 3. | Bw. Ernest N. Kiwale | - | Mkurugenzi wa Manispaa | - | Mjumbe |
| 4. | Bw. Timoth Anyasi | - | Afisa Elimu | - | Mjumbe |
| 5. | Bw. Ulinyelusya Mwamtobe | - | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara | - | Mjumbe |
| 6. | Dr. Ikaji Rashid | - | Mkuu wa Idara ya Afya | - | Mjumbe |
| 7. | Bw. Hissan Ndimbo | - | Mhasibu | - | Mjumbe |
| 8. | Bibi Hellen Peter | - | Kny Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi | - | Mjumbe |
| 9. | Bw. Reuben Elisante | - | Msanifu Majengo | - | Mjumbe |
| 10. | Eng. Pius Mutechura | - | Mkuu wa Idara ya Ujenzi | - | Mjumbe |

### 1.2 WAALIKWA

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Charles Semizigi | - | Afisa Mtendaji Kata ya Vijibweni |
| 2. | Bw. Ricky Paschal | - | Afisa Mtendaji Kata ya Kimbiji |
| 3. | Bw. Nobart Nestory | - | Afisa Mtendaji Kata ya Kigamboni |
| 4. | Bw. Juvenalis Mauna | - | Mkuu wa Idara ya Mazingira na Udhibiti wa Taka ngumu |
| 5. | CPA Chacha Nyamriba | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 6. | Bw. Godfrey Mwangairo | - | Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi |
| 7. | Bw. Mohamed Nyasama | - | Afisa Biashara |
| 8. | Bw. Richard Minja | - | Afisa Mtendaji Kata ya Tungi |
| 9. | Bibi Theophilda Christopher | - | Afisa Mtendaji Kata ya Kisarawe II |
| 10. | Bw. Joseph Barongo | - | Kny Afisa Mtendaji Kata ya Somangila |
| 11. | Bw. Kiwa Ninalwo | - | Afisa Mtendaji Kata ya Mjimwema |

### 1.2 SEKRETARIET

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bibi Juliel Kahembe | - | Mwandishi wa Mikutano |
| 2. | Bw. Felix Baitwa | - | Mwandishi wa Mikutano |

### 2.0 MUHT. NA. KGMC/1/10/2021: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao saa 2:00 asubuhi.

### 3.0 MUHT. NA. KGMC/2/10/2021: KUTHIBITISHA AGENDA

Agenda zifuatazo ziliwasilishwa katika kikao kwa ajili ya majadiliano:-

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kupokea na kujadili utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19
4. Kufunga kikao

Wajumbe walizipokea na walizithibitisha agenda hizo kwa ajili ya majadiliano.

## 4.0 MUHT. NA. KGMC/3/10/2021: KUPOKEA NA KUJADILI UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UVIKO-19

Mratibu wa utekelezaji wa miradi ya UVIKO-19 aliiwasilisha taarifa alieleza kuwa Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu wa Dola za kimarekani milioni 567 sawa na shilingi bilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha la kimataifa (IFM) kwa ajili ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19. Ili kuchangia kufufua uchumi kwa sekta zilizopata athari za kiuchumi kutokana na madhara ya UVIKO -19. kati ya fedha hizo Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeidhinishiwa kupokea jumla ya shilingi bilioni 535.68 ambayo ni sawa na asilimia 41.2 ambapo shilingi bilioni 304 ni kwa ajili ya elimu msingi, shilingi bilioni 223.68 ni kwa ajili ya afya ya msingi na shilingi bilioni 5.00 ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogowadogo/wajasiliamali wakiwemo wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Aidha pamoja na mambo mengine imeelekezwa kutekeleza maelekezo mahsusi yafuatayo:-

- Kuunda Kamati ya Mkoa ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi husika na kuhakikisha kwamba taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo zinawasilishwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kila baada ya wiki mbili.

- Kuhakikisha kila Halmashauri inaunda Kamati ya uratibu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi hiyo

- Kuhakikisha utekelezaji wa miradi unaanza ndani ya wiki mbili mara baada ya fedha kupokelewa
- Kuhakikisha miradi ya ujenzi wa madarasa inakamilika kabla au ifikapo tarehe 15 Desemba, 2021 na miradi mingine ikamilike kabla au ifikapo tarehe 30 Aprili, 2022

- Halmashauri zinaweza kutumia wakandarasi wa ndani au utaratibu wa force account. Hata hivyo mnasisitizwa gharama za utekelezaji kwa kutumia njia yoyote zisizidi makadirio ya fedha zilizotengwa kwa shughuli husika.

- Halmashauri zitakazotaka kufanya mabadiliko ya utekelezaji wa eneo la mradi, maombi yawasilishwe kwa maandishi kwa Katibu Mkuu Ofisi Rais – TAMISEMI ndani ya wiki moja baada ya kupokea fedha hizo

- Viongozi wa mikoa, wilaya na Halmashauri katika kipindi hicho mnaelekezwa kuepuka safari zisizo za lazima zinazohusu kutoka nje yamkoa isipokuwa kwa kibali cha viongozi wakuu wan chi (Mhe Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu)

- Utekelezaji wa miradi yote uzingatie thamani ya fedha na ubora wa miradi

- Watoa huduma wa vifaa na mafundi watangaziwe kazi zilizopo kupitia tovuti za mkoa na Halmashauri pamoja a mbao za matangazo katika ofisi za umma

- Halmashauri zinaenlekezwa kufnaya maunuzi ya paoja (Bulk procurement) ili kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi

- Waheshimiwa Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri pamoja na madiwani wote kupitia kamati zao wahakikishe wanasimamia miradi hiyo kwa kushirikiana na watendaji wa Halmashauri

- Wakurugenzi wa Halmashauri wahakikishe miradi yote iliyokamilika na ununuzi wa vifaa zinawekwa alama ya mpango wa maendeleo kwa ustawi na mapambano dhidi ya UVIKO-19

- Kuhimiza wananchi kushiriki ujenzi wa miradi inayoendelea katika maeneo yao na kutoa taarifa endapo kuna ubadhilifu wa fedha

- Kabla ya kujenga madarasa kwneye vituo shirikishe imeelekezwa kuchukua picha ya hali halisi kabla ya ujenzi wa madarasa mapya kwa ajili ya kumbukumbu za baadaye

- Kwa Halmashauri za Majiji zote, Halmashauri za Manispaa za Kinondoni, Temeke, Ubungo na Morogoro mnaelekezwa kuwasilisha mapendekezo ya mpango wa kuboresha maeneo ya kufnaya biashara ya wafanyabiashara wadogo/ wajasiliamali/wamachinga ili kuweza kutoa fedha hizo

- Utekelezaji wa mpango huo utafanywa kupitia mradi na 5441 ambao unaitwa Tanzania Covid – 19 Social – Economic Response and Recovery Plan (TCRP)

- Kiasi cha fedha ambacho kimeonyeshwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ni kwa ajili ya usimamizi, uratibu na ufuatiliaji wa miradi ya sekta zote katika maeneo ambayo yataratibiwa na Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwenye Halmashauri na Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu kwneye sekretarieti za mkoa

- Fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya huduma za dharura, vifaa vya ICU, X-Ray, magari ya kubebea wagonjwa ambayo yatagawiwa katika Halmashauri zote na magari ya uratibu wa huduma za afya katika mkoa yote utafanywa kwa pamoja kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI

- Kamati zinazoundwa zifuatilie pia miradi inayoendelea kutekelezwa kupita fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti ya

serikali ya mwaka 2021/2022 ikijumuisha fedha za tozo ya miamala ya ismu

- Mamlaka za Serikali za Mitaa zihakikishe ujenzi huo wa madarasa unaendana na ujenzi wa maundu ya vyoo (kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato). Aidha ujenzi wa madarasa utajumuisha ununuzi wa madawati 50 kwakila darasa (Kiti, na meza) kwa shule za sekondari na madawati 16 kwa kila darasa litakalojengwa katika vituo shikizi 970

Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni imepokea shilingi 1,760,000,000/= kama mchanganuo ufuatao unavyoonesha:-

i. Sekta ya sekondari shilingi 680,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 34
ii. Sekta ya msingi shilingi 160,000,000/= kwa ajili ya madarasa (vituo shikizi) 4 na bweni 1
iii. Ununuzi wa mashine ya X-Ray shilingi 420,000,000 hospitali ya wilaya
iv. Afya (uhamasishaji na utoaji wa chanjo) shilingi 43,093,731.63

Utekelezaji utatumia utatumia 'force account'

**MJADALA**

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kujadili kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wa Kamati alieleza kuwa TAMISEMI imeeleza kuwa hadi kufikia tarehe 15/12/2021 ujenzi wa madarasa uwe umekamilika. Aidha ifikapo tarehe 30 Aprili, 2022 miradi mingine iwe imekamilika. Pia alisisiitiza uaminifu katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na uwajibikaji.

Kadhalika, Mwenyekiti alieleza kuwa Kamati mbili zitaundwa kwenye eneo la mradi ambazo ni Kamati ya Ujenzi na Kamati ya Ukaguzi/mapokezi. Kamati ya ujenzi itakuwa na Mwenyekiti ambaye atakuwa Mkuu wa shule, Mhandisi na Kiongozi kutoka kwenye jamii. Aidha kwenye Kamati ya Ukaguzi/mapokezi kutakuwa na kiongozi wa siasa, Afisa Manunuzi na Mhandisi.

Mkurugenzi wa Manispaa alishauri Mhandisi ujenzi aandae dokezo la ununuzi wa vifaa kama vile mabati, nondo. Pia alishauri timu iende kukagua maeneo ya uwekezaji wa miradi hiyo ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa na kuiwasilisha.

Ilielezwa kuwa Wakuu wa Idara wenye miradi waandikiwe barua za utekelezaji ili waweze kuandaa madokezo. Pia kuwepo na majalada ya kutunza kumbukumbu za miradi, iwasilishwe orodha ya mafundi na ununuzi wa matofali uzingatie mashine ya EFD pamoja na manunuzi ya vifaa vingine.

Aidha alishauriwa ushirikiano uwepo katika kutekeleza miradi hiyo. Mkuugenzi alisisitiza Watendaji wa Kata kusimamia miradi vizuri ikiwa ni pamoja na kila mtumishi kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**13.0 MUHT. NA. KGMC/4/10/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 5.45 asubuhi.

............................................
**MWENYEKITI**

............................................
**KATIBU**

**UMETHIBITISHWA**

TAREHE 26/10/2021